

**MWANZA**  
**SENGEREMA DC**  
**SIGNED CONTACTS FOR AWARDED COMPANIES AND THEIR BENEFICIAL OWNERS FOR COVID**  
**-19**

S/N	PROJECT NAME AWARDED AND NATURE OF ACTIVITY (E.g equipment, construction)	NAME OF AWARDED COMPANY	BENEFICIAL OWNERS OF AWARDED COMPANY	VALUE OF THE CONTRACT (TZS)
1	6 Attached classes for primary schoo(madarasa ya shule shikizi)	Force account	wachapakazi group(0762308024,Luhigo Katemi 0787359558)	120,000,000.00
2	129 secondary classes for secondary school	Force account	Kongeja Shija 0762308024	2,580,000,000.00
3	1 dormitories Chifunfu primary school		Ledenatus Mashauri 0689555787	80,000,000.00
4	Machinga martket	Nil	Nil	Nil
5	1 Staff House(3 in one)	Force account	Kongeja Shija 0762308024	90,000,000.00
6	1 EMD	Force account	Kongeja Shija 0762308024	300,000,000.00
7	ICU	Nil	Nil	Nil

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA  
TAREHE 21.11.2021 KWENYE OFISI YA MKUU WA IDARA YA MIPANGO  
KUANZIA SAA 2:35 ASUBUHI HADI SAA 6:24 MCHANA**

**WALIOHUDHURIA**

1. Pastory Mukaruka - Mwenyekiti
2. John Mwita - Katibu
3. Mwita M. Waryuba - Mjumbe
4. Donati M. Bunonosi - Mjumbe

**WAALIKWA**

1. Serapian Matiku -
2. Paschal W. Mafuru

**PMU SEKRETARIATI**

1. Alex K. Tabaro

**AMBAO HAWAKUHUDHURIA KWA TAARIFA**

1. Christina Bunini - Kwa taarifa

**AGENDA ZA KIKAO**

1. Kufungua kikao
2. Kusoma na Kuthibitisha agenda za kikao
3. Kusoma na kuthibitsisha muhtasari wa kikao cha bodi ya zabuni kilichofanyika tarehe 16/10/2021
4. Kuridhia njia ya manunuzi katika miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarsa 129 shule za sekondari, vyumba 6 shule shikizi, jingo 1 la kutolea huduma za dharula, hospitali ya Wilaya ya Sengerema na nyumba 1 wanayokaa watumishi 3

**AGENDA NA.01/21/11/2021**

**KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na kuwaomba kujadili vizuri ajenda za kikao ili maazimio yatakayo kuwa yamefikwa yawe na manufaa kwa Halmashauri. Kikao kilifunguliwa saa 2:35 Asubuhi.

**AGENDA NA.02/21/11/2021**

**KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO**

Mwenyekiti alimkaribisha katibu kuwasomea wajumbe agenda za kikao. Katibu aliwasomea wajumbe agenda a kikao na wajumbe wote kwa kauli moja walilidhia agenda hizo bila nyongeza.

**AGENDA NA.03/21/11/2021**

**KUSOMA NA KUTHIBITSISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 16/10/2021**

Mwenyekiti alimkaribisha katibu kuwasomea wajumbe muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 16/10/2021. Katibu aliwasomea wajumbe muhtasari wa



kikao hicho kurasa kwa kurasa na wajumbe walifanya marekebisho ya kiuchapaji ya muhtasari huo na kisha baada yah apo walikubaliana kwa kauli moja juu ya yote yaliyokuwa yamejadiliwa siku hiyo na ndipo muhasari huo ukathibitishwa na mwenyekiti Pamoja na katibu kwa kuwekwa Saini kama uthibitisho.

**AGENDA NA. 04/21/11/2021**

Kuridhia njia ya manunuzi katika miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarsa 129 shule za sekondari,vyumba 6 shule shikizi,jingo 1 la kutolea huduma za dharula,hospitali ya Wilaya ya Sengerema na nyumba 1 wanayokaa watumishi 3 Wajumbe walitaarifiwa kuwa Halmashauri imepata fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya ujenzi wa madarasa 129 ya sekondari,6 shule shikizi,jingo moja la kutolea huduma za dharula na nyumba 1 ya mtumishi katika kituo cha Afya Kagunga vijengwe kwa njia ya force account.Wajumbe wote walikubaliana kwa hoja hiyo na kushauri kuwa ujenzi uanze mara moja kukimbizana na muda.

**AGENDA NA.11/21/11/2021**

**KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote waliohudhuria kwenye kikao hicho kwa michango yao katika agenda zote zilizojadiliwa tangu mwanzo wa kikao hicho na kisha alifunga kikao saa 6:24 Mchana.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA;**

**MWENYEKITI**



.....

**TAREHE**

**KATIBU**

